

Kuleta Usawa

Kikundi cha Uzima kilianza kwenye jumuiya jina la utani 'Kanda ya Maovu'. Baada ya mwaka Kikundi cha Uzima kiliomba maalum kwa watu wanaojulikana kuanzisha fujo kwenye eneo. Siku moja waliwakaribisha watu hao kwenye kikundi chao. La kushangaza kwenye mwaliko, wenye kuanzisha fujo walikuja na kwa muda wakajenga urafiki na wanachama wa Kikundi cha Uzima. Hii iliwaongoza kwa Yesu na walipompa Yesu maisha yao, alianza kubadilisha maisha yao! Matokeo, uovu ukashuka na tabia ya kijiji chao ilibadilika kabisa!

Huu ni mfano wa wanachama wa Kikundi cha Uzima wakisimamia usawa na kuleta mabadiliko kwenye jumuiya. Huu ni moyo mzuri wa kumfuata Yesu. Kama Wakristo hatuwezi tu kupuuzia hoja kwenye maeneo yetu na dunia inayotuzunguka. Mungu wetu ni Mungu anayejali kwa undani juu ya usawa. Anatumka sisi, watu wake, kusimamia usawa na kusaidia kuponya dunia hii iliyoharibika.

Dunia imejaa mambo yasiyo sawa. Tunaishi kwenye dunia ya vurugu, vita, njaa na umaskini uliyo kidhiri. Watu wanakabiliana na mateso kwa rangi zao, imani na wanachoamini. Kila siku watu wananyoywa, kuibiwa kutoka na kuuzwa utumwani. Watu kwa ujumla wanateseka na matukio ya misiba, magonjwa na mabadiliko ya hali ya hewa. Dunia siyo namna Mungu alivyotaka iwe.

Mungu siku zote ametutaka sisi, watoto wake, kuwa sehemu ya jibu. Yesu alisimama kwa waliokuwa wapeke, waliodidimizwa, na kutengwa. Tunapaswa kufanya hivyo. Matayo 25:40 Yesu alisema, "Na Mfalme atajibu, akiwaambia, Amin, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi."


Fikiri juu ya watu kwenye eneo lako. Jumuiya yako itaonekanaje kama utawaona watu hawa kwa jinsi unavyomwona Yesu? Je utakuwa unawahudumia kwa namna hiyo? Je utavumilia uonevu usiyo sawa kwenye jamii yako? Je utakaa nyuma na kuangalia watu wakibaguliwa na kuibiwa? Hii ndiyo changamoto halisi kubwa kwa Yesu. Kama tunasema tunampenda Yesu, ni lazima kuonyesha upendo huo kwa wapeke, waliodidimizwa na waliotengwa. Sehemu ya upendo huo ni kusimama kinyume na uonevu usiyo sawa wanayokabiliana nayo. Wote tunajua matatizo yaliyomo kwenye maeneo yetu na kama Kikundi cha Uzima kwenye hadithi, utakuwa sehemu ya majibu ya Mungu kwa matatizo haya.

Zingatia!

Je ni matendo gani makubwa yasiyo sawa yamo kwenye jumuiya yako? Inawezekana ni mtu fulani anayeonewa, au kikundi cha watu kinachotendewa vibaya. Wiki ijayo, kutana pamoja na Wakristo wengine na kuyaombea mazingira haya ambayo Mungu ameweka moyoni mwako. Chukua muda kufikiri juu ya hatua unazopaswa kuchukua ili ufanye jambo fulani juu yake.


Omba:

- 1) Mungu atakuonyesha mazingira ambayo hakuna usawa kwenye jumuiya yako.
- 2) Roho Mtakatifu atakupa ujasiri na hekima kutenda jambo kwa namna ya kuleta usawa.



"Oo utukufu kwa Mungu. Leo tumeanzisha Kikundi cha Uzima ndani ya moja ya magereza yetu ya Kenya kwa wafungwa ambao tutawaandaa kuongoza Vikundi vya Uzima kwenye jumuiya zao watakapotoka magereza. Nimeanzisha Kikundi cha Uzima na wafungwa nane.

- Beatrice, Nairobi, Kenya



Somo hili lilichukuliwa toka "Maneno Hayatoshi" limechukuliwa toka "Penda Kijiji Chako"

Kwa maelezo zaidi:

dignityonline.org.uk/publications